



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA MANISPAA YA LINDI



Kumb. Na. LMC/J.20/3 VOL III/72

09/10/2023

## TANGAZO LA AJIRA

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Lindi anayo furaha kutangaza nafasi ya Ajira ya kudumu kwa Watanzania wenye sifa na nia ya kufanya kazi katika Halmashauri ya Manispaa ya Lindi kuomba kazi ya Udereva Daraja la II.

### 1.0. DEREVA DARAJA LA II NAFASI (1)

#### 1.1. SIFA ZA MWOMBAJI

Mwombaji anatakiwa awe na sifa zifuatazo:-

- a) Awe amehitimu kidato cha (IV) au cha (VI) na kufaulu.
- b) Awe na Leseni Daraja la C au E ya uendeshaji wa magari, ambaye amefanya kazi kwa muda uziopungua mwaka Mmoja bila kusababisha ajali.
- c) Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na Chuo cha VETA au NIT au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

#### 1.2. MSHAHARA

Ngazi ya Mshahara ni TGS B kwa mwezi.

#### 1.3. Kazi na majukumu:-

- i. Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kugundua ubovu unaohitaji matengenezo.
- ii. Kuwepeleka watumishi mbalimbali kwenye safari za kikazi.
- iii. Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari.

Ofisi ya Mkurugenzi, Halmashauri ya Manispaa ya Lindi, S.L.P 1070 Lindi, Simu: +255 023-220-2184,  
Nukushi: +255 023-220-2116, Barua pepe: info@lindimc.go.tz, Tovuti: www.lindimc.go.tz

- iv. Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali.
- v. Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari na
- vi. Kufanya usafi wa gari.

#### MASHARTI YA JUMLA

- i. Waombaji wote wawe Raia wa Tanzania.
- ii. Waombaji wote wawe na Umri kati ya miaka 18 – 45.
- iii. Waombaji wote waambatishe nakala ya cheti cha kuzaliwa.
- iv. Waombaji waambatishe nakala ya cheti cha kuzaliwa.
- v. Waombaji waambatishe maelezo binafsi (CV) yenye anuani na namba za simu za kuaminika na majina mawili (2) ya Wadhamini.
- vi. Maombi yote yaambatishe na picha moja (Passport size ya hivi karibuni na iandikwe jina kwa nyuma).
- vii. Waombaji wote waambatishe nakala za vyeti vya Taaluma/Shule na vyeti vya kuhitimu mafunzo ya vyuo.
- viii. Waombaji wote waambatishe nakala ya Kitambulisho cha Taifa (NIDA) kwa ambao hawana Vitambulisho hivyo, namba za NIDA ziandikwe kwenye maelezo binafsi (CV).
- ix. Maombi yote yatakayoambatanishwa na taarifa ya matokeo ya Kidato cha NNE au Sita (Result Slip) hayatafanyiwa kazi.
- x. Watakao chaguliwa kufanya usaili watajulishwa tarehe mahali utakapofanyika usaili kupitia tovuti ya Halmashauri, Mbao za Matangazo na kupigiwa simu.
- xi. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 23/10/2023.

#### UTARATIBU WA MAOMBI

Maombi yote yatamwe kwa Anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi wa Halmashauri,  
Halmashauri ya Manispaa,  
S. L. P 1070,  
LINDI.

  
Juma A. Mwele  
MKURUGENZI WA MANISPAA  
HALMASHURI YA MANISPAA  
LINDI.



Ofisi ya Mkurugenzi, Halmashauri ya Manispaa ya Lindi, S.L.P. 1070 Lindi, Simu: +255 023-220-2164,  
Nukushi +255 023-220-2116. Barua pepe: info@lindimc.go.tz. Tovuti: www.lindimc.go.tz